# GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

*(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)*

**Sehemu ya CXXXI Nam. 6994** **17 JUNI , 2022** **Bei Shs. 3000/=**

*Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti* *Hutolewa kila Ijumaa*

**YALIYOMO** Ukurasa

Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar, Nam. 7 ya 2014
Kanuni za Tozo za Huduma na Biashara za Baraza, 2022
[Chini ya kifungu vya 27(1) (c) ]..................................................................347

**SEHEMU YA SHERIA**

Tangazo la sheria lililotajwa hapo chini limetangazwa katika Gazeti Rasmi hili

Tangazo la Sheria.

Nam: 100 :- Kanuni za Tozo za Huduma na Biashara za Baraza, 2022

---

**SHERIA YA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA ZANZIBAR NAM. 7 YA 2014**

---

**KANUNI ZA TOZO ZA HUDUMA NA BIASHARA ZA BARAZA, 2022**

**[Chini ya kifungu cha 27(1) (C)]**

---

**MPANGILIO WA KANUNI**

**KANUNI:** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Ufafanuzi.



CamScanner

**SEHEMU YA PILI**
**UHIFADHI WA MAZINGIRA NA UKUSANYAJI WA TAKA**

3. Usafi wa Mazingira.
4. Wajibu wa Ukusanyaji na Utupaji taka.
5. Malipo ya usafi wa mazingira katika Eneo.

**SEHEMU YA TATU**
**UKAGUZI WA AFYA, MIPANGO MIJI NA LESENI**

6. Ukaguzi wa Afya.
7. Ukaguzi wa Ujenzi.
8. Ukaguzi wa Leseni.

**SEHEMU YA NNE**
**HUDUMA ZA USIMAMIZI WA VITUO VYA DALADALA**

9. Vituo vya Daladala.

**SEHEMU YA TANO**
**MAEGESHO YA VYOMBO VYA MOTO**

10. Maegesho ya vyombo vya moto.
11. Vyombo vitakavyo samehewa kufanya malipo.
12. Baraza kutokua na dhamana ya uharibifu.

**SEHEMU YA SITA**
**UTOWAJI WA LESENI ZA BIASHARA**

13. Ukataji wa leseni ya biashara.
14. Kusitishwa kwa leseni ya biashara.
15. Kufutwa kwa leseni biashara.
16. Kupotea kwa leseni ya biashara.
17. Upekuzi na ufatiliaji wa leseni.
18. Adhabu za makosa ya leseni.
19. Tangazo la Biashara.
20. Ada ya mnada.
21. Ukodishwaji wa kizimba.
22. Uanikaji na uondoshaji wa dagaa.
23. Uingizaji na ushushaji wa mkaa.
24. Uingizaji na ushushaji wa mbao.
25. Huduma za vyoo.
26. Biashara ndogo ndogo

**SEHEMU YA SABA**
**ADA ZITOKANAZO NA KODI AU PANGO**

27. Taarifa ya kukodishwa mali zinazohamishika na zisizohamishika.
28. Mkodishaji wa ardhi kwa ujenzi wa mnara.
29. Ada ya ujenzi mnara na uendeshaji.

CS CamScanner

**TANGOZO 71**

## SHERIA YA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA ZANZIBAR NAM. 7 YA 2014

---

## KANUNI ZA TOZO ZA HUDUMA NA BIASHARA ZA BARAZA, 2022

**[Chini ya kifungu cha 27(1) (C)]**

---

**KWA UWEZO** lililopewa chini ya kifungu cha 27(1) (C) cha Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar Nam.7 ya 2014, Baraza linatunga Kanuni zifuatazo:

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Tozo za Huduma na Biashara za Baraza, 2022 na zitaanza kutumika mara baada ya kusainiwa na Meya na Mkurugenzi na kuchapishwa katika Gazeti rasmi la Serikali.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Ada" maana yake ni fedha inayotozwa kwa ajili ya kupewa huduma katika eneo la Baraza;

"Afisa dhamana" maana yake ni Afisa yeyote wa Baraza atakayeidhinishwa na Mkurugenzi kwa ajili ya kufanya kazi maalum;

"Afisa Mkaguzi" ni afisa anayekagua biashara au eneo;

"Afisa Mpekuzi" ni Afisa anayefanya upekuzi na ufatiliaji wa maeneo ya biashara ili kubaini makosa;

"Baraza" maana yake ni Baraza la Manispaa ya Magharibi "A";

"Beji" maana yake ni kitambulisho kinachotolewa na Baraza chenye lengo la kuwatambua wajasiriamali wa Wilaya ya Magharibi "A";

"Biashara ndogo ndogo" maana yake ni biashara zote ambazo kisheria hazihitaji leseni zinazofanyika ndani ya eneo la Baraza katika maeneo yaliyoruhusiwa kisheria;

"Daladala" maana yake ni gari za biashara zenye kuchukua abiria aidha kutoka Mjini au shamba;

"Eneo" maana yake ni sehemu ya mamlaka ya Eneo la Manispaa ya Magharibi "A" kama ilivyotangazwa na Waziri kuwa ni Wilaya ya Magharibi "A" kwa mujibu wa Sheria Nam.8 ya 2017;

CS CamScanner

"Gharama" maana yake ni ada inayotokana na aina ya biashara;

"Kaya" maana yake ni mtu au kundi la watu wanaoishi mahali pamoja kama familia;

"Kibali" maana yake ni kitambulisho cha ruhusa kinachotolewa na Baraza kwa ajili ya kazi maalum;

"Kizimba" maana yake ni meza au vibaraza vinavyotumika kufanyia biashara kupitia soko au masoko;

"Maeneo ya wazi" inajumuisha sehemu yoyote iliyokuwa haimilikiwi na mtu yeyote, hivyo sehemu hiyo itakuwa ipo chini ya Baraza;

"Maliasili zisizorejesheka" inajumuisha mawe, kokoto, mchanga, udongo, matofali ya kuchonga kifusi na maliasili zinazofanana na hizo;

"Mamlaka" maana yake ni Baraza;

"Masaa ya udhibiti" maana yake ni masaa ambayo wahusika wa eneo wanakuwepo;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Baraza anayeteuliwa chini ya kifungu cha 39(1) cha Sheria;

"Mnara" maana yake ni chombo kilichojengwa kwa madhumuni ya kupokea au kurejesha mawasiliano ya habari;

"Mtu" inajumuisha mtu binafsi, Shirika, Kampuni au Taasisi;

"Vyombo" inajumuisha vyombo vyote vya usafiri wa barabarani na baharini;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, Kampuni, Shirika au Taasisi inayofanya kazi kwa ajili ya kumuwakilisha muajiri wake ambae ni Baraza;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

## SEHEMU YA PILI
## UHIFADHI WA MAZINGIRA NA UKUSANYAJI WA TAKA

Usafi wa Mazingira.

**3.** Bila ya kuathiri Sheria zinazohusiana na Mazingira na sheria nyengine, Baraza lina wajibu wa kuhakikisha mazingira yote ya eneo kuwa ni safi.

Wajibu wa Ukusanyaji na Utupaji taka.

**4.-**(1) Katika kutekeleza wajibu wake kama ilivyoainishwa katika kanuni ya 3 ya Kanuni hizi, Baraza au Wakala atakuwa na wajibu wa uchukuaji na utupaji wa taka zote zilizomo ndani ya eneo.

(2) Mwananchi atakua na wajibu wa kuweka mazingira yake safi na kuzipeleka taka sehemu iliyotengwa na Baraza kuanzia saa moja asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni.

CS CamScanner

(3) Mtu yeyote ambaye atapewa huduma ya ukusanyaji na utupaji wa taka katika eneo atafuata maelekezo ya Baraza katika kufanya kazi hizo.

(4) Mtu yeyote hatotoa huduma ya uchukuwaji na utupaji wa taka kwa kupata malipo bila ruhusa ya Baraza.

(5) Endapo mtu yeyote atakwenda kinyume na kanuni ndogo ya (2) na (3) ya kanuni hii, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini ya Shilingi Elfu Hamsini za Kitanzania kwa mtu mmoja au kifungo kisichozidi wiki mbili, kwa Taasisi faini ya Shilingi Laki Tano za Kitanzania kwa kosa la kwanza na ikirudia kosa itatozwa Shilingi Milioni Moja za Kitanzania.

(6) Kila mfanyabiashara katika eneo atahifadhi bidhaa zake anazoziuza kwa unadhifu na kuzingatia masharti ya usalama wa afya kwa watumiaji.

(7) Mfanyabiashara yeyote atakayeshindwa kuhifadhi biashara yake atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini ya Shilingi Elfu Hamsini za Kitanzania au kifungo cha kipindi cha wiki mbili.

Malipo ya usafi wa mazingira katika Eneo.

**5.-**(1) Baraza au wakala kwa kutumia njia maalumu ya ukusanyaji wa fedha, atakusanya fedha kutoka kila kaya katika eneo kwa ajili ya malipo ya usafi wa mazingira.

(2) Kila mmiliki wa nyumba ataonyesha idadi ya kaya ambazo zinaishi katika nyumba yake na pale ambapo wanahama atatoa taarifa kwa Baraza.

(3) Kila kaya au nyumba italipa ada ya usafi wa mazingira kama itakavyoainishwa katika Jadweli la Kwanza la Kanuni hizi.

(4) Nyumba au kaya itakayoshindwa kulipa ada ya taka kwa mwezi husika gharama zitaongezeka kutoka Shilingi Elfu Tatu mpaka Shilingi Elfu Tano.

(5) Mtu yeyote atakayeshindwa kulipa ada ya usafi kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (3) ya kanuni hii bila kutoa taarifa yoyote ya kimaandishi kwa Baraza kwa muda wa miezi minne (4) mfululizo, atakua ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini ya Shilingi Elfu Hamsini za Kitanzania.

(6) Mtu yeyote atakayefanya biashara katika eneo, atalipa gharama za usafi wa mazingira kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Kwanza la Kanuni hizi na iwapo atashindwa kufanya malipo hayo kutakuwa na ongezeko la Shilingi Laki Mbili za Kitanzania.

(7) Mtu yeyote atakayeshindwa kulipa ada ya usafi kwa mujibu wa Kanuni ndogo ya (5) ya kanuni hii bila kutoa taarifa yoyote ya maandishi kwa Baraza kwa muda wa miezi mine (4) mfululizo, atakua ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa ada hiyo pamoja na asilimia 20% ya ziada ya gharama za usafi wa mazingira.

## SEHEMU YA TATU
## UKAGUZI WA AFYA, MIPANGO MIJI NA LESENI

Ukaguzi wa Afya.

**6.-**(1) Bila ya kuathiri sheria ya usimamizi wa afya, Baraza lina wajibu wa kufanya ukaguzi katika makaazi ya watu na maeneo ya biashara.

CS CamScanner

(2) Mtu yeyote anaefanya shughuli zake za kiuchumi na kijamii ndani ya eneo la Baraza atawajibika kulipa ada ya ukaguzi kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Kwanza la Kanuni hizi.

(3) Mfanyabiashara atatoa taarifa juu ya biashara yake na kufanyiwa ukaguzi kabla ya kuanza kufanya biashara hiyo.

(4) Mfanyabiashara atapima afya na kupatiwa vyeti vya afya kwa mujibu wa Sheria ya Ukaguzi na Kanuni za afya.

(5) Kila mfanyabishara atawajibika kuviweka vyeti vya afya katika sehemu anayofanyia biashara.

(6) Mfanyabiashara atawajibika kuvaa vazi maalum wakati wa kufanya biashara yake.

(7) Mfanyabiashara yeyote atakayeshindwa kutoa mashirikiano kwa maafisa ukaguzi au kufuata miongozo ya afya, atakua ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini ya Shilingi Laki Moja za Kitanzania au kifungo cha wiki mbili.

Ukaguzi wa Ujenzi.

**7.** Mtu yeyote anayetaka kuomba kibali kwa ajili ya ujenzi atajaza fomu ya ukaguzi wa eneo analotaka kujenga.

Ukaguzi wa Leseni.

**8.** Baraza litafanya ukaguzi kwa biashara zote wakati wa maombi ya leseni na mfanyabiashara atalipia ada ya ukaguzi kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Pili la Kanuni hizi.

## SEHEMU YA NNE
## HUDUMA ZA USIMAMIZI WA VITUO VYA DALADALA

Vituo vya Daladala.

**9.-**(1) Bila ya kuathiri Sheria nyingine yoyote, Baraza litajenga, litaimarisha na litavisimamia vituo vya daladala katika eneo.

(2) Mtu yeyote anayefanya shughuli za biashara ya usafirishaji wa abiria kwa daladala, atafika katika kituo na kulipia ada kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Kwanza la Kanuni hizi.

(3) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na Kanuni ndogo ya (2) ya Kanuni hii atakua ametenda kosa na ikithibitika atalipa ada iliyopangwa katika kifungu kidogo cha (2) cha kanuni hii na faini ya Shilingi za Kitanzania.

(4) Mtu yeyote atakaeharibu, kuchora au kuvunja vituo vya daladala atakua ametenda kosa na akitiwa hatiani atarekebisha sehemu au eneo aliloharibu na atalipa faini isiyopungua Shilingi Laki Saba za Kitanzania na akishindwa kurekebisha na kulipa faini atatumikia kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu.

## SEHEMU YA TANO
## MAEGESHO YA VYOMBO VYA MOTO

Maegesho ya vyombo vya moto.

**10.-**(1) Baraza litakuwa na maegesho kwa ajili ya vyombo.

(2) Baraza linaweza kumpa mamlaka wakala wake kuanzisha sehemu maalum kwa ajili ya huduma ya kuegesha vyombo na malipo yake yataamuliwa na Mamlaka kwa mujibu wa makubaliano watakayokubaliana.

CamScanner

(3) Baraza au wakala aliyeidhinishwa anaweza kuweka alama maalumu kwa ajili ya kutoa maelekezo ya namna ya kuweka chombo katika egesho.

(4) Mtu yeyote atakaegesha chombo kwa muda atalipa ada ya uegeshaji kama itavyoainishwa katika Jadweli la kwanza la Kanuni hizi.

(5) Baraza litampatia mteja risiti ya malipo kwa huduma ya egesho ambayo itaonyesha kiwango cha ada ya huduma na muda wa chombo uliotumika katika eneo hilo.

(6) Mtu yeyote atakayekiacha chombo katika sehemu ya kuegesha vyombo ndani ya masaa ya udhibiti kwa kipindi kinachozidi wakati ulioruhusiwa, msimamizi wa mahali hapo atamtoza mmiliki wa chombo malipo ya kawaida na malipo ya ziada kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Kwanza Kanuni hizi.

(7) Mtu yeyote atakayeegesha chombo katika sehemu isiyo rasmi atakua ametenda kosa na atalipa mara mbili ya ada ya egesho.

(8) Mtu yeyote atakayeegesha au kulaza chombo na akakataa kulipa ada ya huduma ya maegesho au kulaza chombo au akaegesha au kulaza gari zaidi ya muda alioruhusiwa kutokana na ada aliolipa atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Laki Moja za kitanzania pamoja na kulipa ada anayodaiwa.

(9) Mtu yeyote atakayeweka chombo cha usafiri na kuchukua nafasi katika eneo la egesho lililotengwa kwa ajili ya maegesho atalipia nafasi yote aliyoitumia kwa ajili ya egesho hilo.

(10) Mtu yeyote atakayeweka mzigo katika eneo la maegesho atakua ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi Laki Moja na Elfu Hamsini za Kitanzania.

(11) Mtu yeyote:

(a) atakaefanya shughuli yoyote inayoleta uchafuzi wa mazingira katika eneo la egesho la vyombo vya usafiri;

(b) atakayefanya shughuli za ufundi mekanika katika eneo la kuegesha magari; au

(c) atakayeondosha alama au vifaa vya maegesho bila ya ruhusa,

atakua ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi Laki Mbili za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Laki Tatu za Kitanzania au kifungo kisichopungua miezi mitatu, na kulipa gharama ya uharibifu wa vifaa vinavyotumika katika eneo la egesho la vyombo.

Vyombo vitakavyo samehewa kufanya malipo.

**11.** Vyombo vifuatavyo vinaweza kuegeshwa katika sehemu za kuegesha vyombo ndani ya masaa ya udhibiti bila ya malipo:

(a) vyombo vya usafiri wa Viongozi wenye hadhi ya Ubalozi;

(b) magari ya kuchukulia wagonjwa;

CamScanner

(c) magari ya Serikali au miradi ya Serikali; na

(d) chombo cha usafiri kwa matukio ya dharura au operesheni ya uokozi.

Baraza kutokua na dhamana ya uharibifu.

**12.** Baraza halitokuwa na dhamana juu ya uharibifu wowote wa chombo cha usafiri utakaotokea maeneo ya kuegesha.

## SEHEMU YA SITA
## UTOWAJI WA LESENI ZA BIASHARA

Ukataji wa leseni ya biashara.

**13.-**(1) Bila ya kuathiri Sheria zinazosimamia utoaji wa leseni, Baraza litakuwa na wajibu wa kutoa huduma za leseni kwa mtu mwenye kukidhi vigezo vya biashara.

(2) Mtu yeyote anayetarajia kufanya biashara atalipia fomu ya maombi na kuijaza, pamoja na kuirejesha ikiwa imeambatanishwa na ada ya leseni kwa mwaka kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Pili la Kanuni hizi.

(3) Pamoja na vigezo vyengine vilivyotajwa katika Kanuni hii, leseni ya biashara haitatolewa ikiwa mtu hajatimiza au hana mambo yafuatayo:

(a) kitambulisho cha mzanzibari au mtanzania au Hati ya Kusafiria;

(b) taarifa za eneo la biashara na utambulisho wa Manispaa;

(c) mkataba ikiwa si mmiliki wa eneo la biashara; na

(d) ada ya usafi.

(4) Mmiliki wa biashara atatoa taarifa ya kutoendelea na biashara ikiwa hana nia ya kuendelea na biashara katika eneo alilolipatia leseni ya biashara.

(5) Mmiliki wa biashara ataiweka leseni sehemu inayoonekana katika eneo la biashara.

(6) Kushindwa kutekeleza masharti ya Kanuni ndogo ya (4) ya Kanuni hii, Mmiliki wa Biashara atalipa ada ya leseni kwa muda wote ambao hakutoa taarifa za kusitisha biashara.

(7) Kila baada ya miezi kumi na mbili mmiliki wa biashara atafanya uhuishaji wa leseni kama itakavyoelekezwa katika Jadweli la Pili.

(8) Mmiliki wa biashara atakaposhindwa kufanya uhuishaji wa leseni ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kuisha muda kwa leseni ya awali atalipa faini kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

Kusitishwa kwa leseni ya biashara.

**14.** Baraza linaweza kusitisha matumizi ya leseni iwapo:

(a) leseni iliyotolewa na Mamlaka husika imemaliza muda wake na haijahuishwa;

(b) mfanyabiashara ameomba kusitisha biashara yake;

(c) atashindwa kutekeleza maelekezo aliyopewa na Baraza;

(d) mfanyabiashara atabadilisha matumizi ya leseni alioruhusiwa na Baraza; na

CamScanner

(e) mfanyabiashara atakiuka utekelezaji wa Kanuni hizi au Sheria nyenginezo zilizopo nchini.

Kufutwa kwa leseni ya biashara.

**15.** Baraza linaweza kufuta matumizi ya leseni iwapo:

(a) mfanyabiashara amekwenda kinyume na masharti yaliyowekwa katika kufanya biashara hiyo;

(b) mfanyabiashara ameitoa leseni yake na kumpa mtu mwengine kuitumia;

(c) mfanyabiashara atadanganya au atatoa taarifa za uongo kwa Baraza katika utaratibu wa ukataji na upatikanaji wa leseni; na

(d) mfanyabiashara atafanya uharibifu katika hati ya leseni ya biashara.

Kupotea kwa leseni ya biashara.

**16.** Mtu yeyote atakayepoteza leseni yake kwa njia moja au nyengineyo anatakiwa:

(a) kutoa taarifa kituo chochote cha polisi;

(b) kutoa taarifa katika ofisi ya Baraza na kueleza sababu za kupotea kwa Leseni hiyo; na

(c) kujaza fomu ya kuombea leseni na kulipa malipo ya asilimia hamsini 50% ambayo ni thamani ya leseni yake ya mwanzo.

Upekuzi na ufatiliaji wa leseni.

**17.-**(1) Baraza au wakala anaweza kufanya upekuzi na ufatiliaji muda wowote katika maeneo ya Baraza ili kuhakikisha masharti na sheria zote yanafuatwa ipasavyo.

(2) Afisa mpekuzi anatakiwa kujaza fomu maalumu juu ya kile alichokipekua na kukigundua kutokana na upekuzi alioufanya.

(3) Mfanyabiashara analazimika kutoa ushirikiano wa kutosha kwa afisa mpekuzi na mfatiliaji.

(4) Mfanyabiashara yeyote atakayekataa kutoa ushirikiano, kufanya udanganyifu, kutumia lugha chafu kwa afisa mpekuzi, au kumfukuza afisa mpekuzi atakua ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini ya Shilingi Laki Moja za Kitanzania au kifungo kwa kipindi cha miezi miwili au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Adhabu za makosa ya leseni.

**18.-**(1) Mtu yeyote atakayefanya biashara zake bila ya kuwa na leseni atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalazimika kukata leseni na kulipa faini isiyozidi Shilingi Laki Tano za Kitanzania na isiyopungua Shilingi Laki Mbili za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu (3) au adhabu zote mbili kwa pamoja.

(2) Mtu yeyote atakayedanganya au katoa taarifa za uongo katika kupata leseni atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi Laki Nne za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Laki Tano za Kitanzania.

(3) Mtu yeyote atakayefanya biashara kwa kutumia leseni ya mtu

CamScanner

mwengine atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyozidi Shilingi Laki Tano na Elfu Hamsini za Kitanzania na isiyopungua Shilingi Laki Nne na Hamsini Elfu za Kitanzania.

(4) Mtu yeyote atakayeshindwa kumpa afisa mpekuzi leseni yake ya biashara wakati wa upekuzi atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi Laki Moja na Elfu Hamsini za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Laki Mbili za Kitanzania.

(5) Mtu yeyote atakayeshindwa kuhuisha leseni ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kumaliza muda wake atakua ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini ya asilimia ishirini 20% ya thamani ya ada ya leseni yake kwa kila mwezi aliozidisha bila ya kuhuisha leseni.

Tangazo la Biashara.

**19.-**(1) Baraza litaweka sehemu maalumu kwa ajili ya matangazo ya biashara.

(2) Mtu yeyote anakayetaka kuweka, kusambaza na kutangaza biashara atakata kibali kutoka Baraza kulingana na ukubwa na aina ya tangazo.

(3) Kibali kitatolewa kwa malipo ya siku au mwaka kulingana na ukubwa, ubora au muonekano wa tangazo kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Huduma zinazotolewa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

(4) Mfanyabiashara yeyote atakaekwenda kinyume na Kanuni ndogo ya (1), (2) na (3) ya Kanuni hii, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa ada ya tangazo na faini ya asilimia hamsini (50%) ya malipo ya kibali au gharama aliyotakiwa kukilipia.

Ada ya mnada.

**20.-**(1) Kutakua na kibali maalumu kwa waendesha minada wote katika masoko ya eneo la Baraza.

(2) Mtu yeyote anayetaka kuendesha mnada katika masoko ya eneo la Baraza atalipia ada ya kibali cha mnada ambayo ni Shilingi Laki Moja za Kitanzania kwa mwaka ambayo anaweza kulipa kwa awamu nne.

(3) Mtu yeyote anayenadishiwa bidhaa yake katika eneo anatakiwa alipe ada ya mnada asilimia tano (5%) ya bidhaa iliyouzwa.

Ukodishwaji wa kizimba.

**21.-**(1) Kutakua na kizimba katika masoko madogo ambayo yatasimamiwa na Baraza.

(2) Kizimba kilichokuwepo kwa mujibu wa Kanuni ndogo ya (1) ya Kanuni hii, kitakodishwa kwa bei itakayoelekezwa na Baraza kwa kuzingatia maeneo.

(3) Mtu yeyote aliyekodi kizimba atakuwa na kitambulisho cha wajasiriamali.

(4) Mtu yeyote aliyekodi kizimba atalipia ada ya usafi kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Kwanza la Kanuni hizi.

Uanikaji na uondoshaji wa dagaa.

**22.-**(1) Kutakuwa na maeneo maalum yatakayotengwa na Baraza kwa ajili ya shughuli za uanikaji wa dagaa.

CamScanner

(2) Mtu yeyote ambaye atataka kufanya shughuli za uanikaji wa dagaa atalazimika kuwa na kitambulisho cha wajasiriamali wadogo.

(3) Kutakua na viwanja vya uanikaji wa dagaa vitavyotengwa na Baraza ambavyo vitakodishwa kwa waanikaji wa dagaa kwa gharama kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Pili la Kanuni hizi.

(4) Kutakua na vibanda katika maeneo ya uanikaji wa dagaa ambavyo vitakodishwa kwa wakaushaji wa dagaa kwa gharama kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Pili la Kanuni hizi.

(5) Mtu yeyote anayetaka kutoa dagaa atalipia gharama za utoaji bidhaa kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Pili la Kanuni hizi.

(6) Mtu yeyote ambaye atajishughulisha na shughuli za uwakala wa uuzaji wa dagaa lililokaushwa atalipia kibali cha uwakala kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Pili la Kanuni hizi.

Uingizaji na ushushaji wa mkaa.

**23.-**(1) Baraza katika kutekeleza jukumu lake litakuwa na wajibu wa kufuatilia namna gani mkaa unaingia na kutoka katika eneo lililotengwa.

(2) Mtu yeyote ambaye atafanya biashara ya kusafirisha na kushusha mkaa atafuata maelekezo kutoka kwa afisa dhamana wa sehemu hiyo.

(3) Baraza au wakala kwa kutumia njia maalumu ya ukusanyaji wa ada ya mkaa, litakusanya ada hiyo kwa kila polo au gunia la mkaa kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Pili la Kanuni hizi.

(4) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na Kanuni ndogo ya (1), (2) na (3) ya Kanuni hii, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini ya Shillingi Laki Moja za Kitanzania au kifungo cha wiki 2.

Uingizaji na ushushaji wa mbao.

**24.-**(1) Baraza au wakala atawajibika kufuatilia mwenendo mzima wa uingizaji na ushushaji wa Mbao katika Eneo.

(2) Mtu atakuwa na wajibu wa kutoa taarifa juu ya uingizaji na ushushaji wa mbao kwa afisa aliyeidhinishwa na Baraza.

(3) Ni jukumu la mfanyabiashara kulipa ada ya uingizaji na ushushaji wa Mbao kwa Baraza kama ilivyoainishwa katika Jadweli la pili la kanuni hizi.

(4)Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na Kanuni ndogo ya (1), (2), na (3) ya Kanuni hii, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini ya Shilling Laki Moja za Kitanzania au kifungo cha wiki 2.

Huduma za vyoo.

**25.-**(1) Baraza litatenga sehemu maalumu kwa ajili ya huduma za vyoo katika maeneo yake.

(2) Mtu yeyote atawajibika kulipia ada ya usafi wa vyoo katika eneo husika kama itakavyoainishwa katikae Jadweli la Kwanza la Kanuni hizi.

CamScanner

Biashara ndogo ndogo.

**26.-**(1) Mtu yeyote anayefanya biashara ndogo ndogo zilizoainishwa katika Jadweli la Pili la Kanuni hizi ndani ya eneo la Baraza atalipa ada ya usajili na kupatiwa kitambulisho maalumu kutoka katika eneo analofanyia biashara.

(2) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na kanuni hii atakuwa ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiopungua Shilingi Laki Tatu za Kitanzania au kifungo kisichopungua miezi mitatu.

## SEHEMU YA SABA
## ADA ZITOKANAZO NA KODI AU PANGO

Taarifa ya kukodishwa mali zinazo-hamishika na zisizo-hamishika.

**27.-**(1) Baraza lina jukumu la kupokea na kusajili taarifa za ukodishwaji wa mali zinazohamishika na zisizo hamishika.

(2) Mmiliki wa mali inayopangishwa atalipa asilimia tano (5%) ya pato la kodi ikiwa ni ada ya ukodishaji wa mali inayohamishika au isiyohamishika katika eneo.

(3) Iwapo mmiliki wa mali iliyopangishwa atashindwa kulipa ada hiyo atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi Laki Tano za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Laki Nane za Kitanzania au kutumikia kifungo kwa muda usiopungua miezi minne.

Mkodishaji wa ardhi kwa ujenzi wa mnara.

**28.-**(1) Baraza linamtaka mtu yeyote atakayekodisha sehemu ya ardhi kwa ajili ya ujenzi wa mnara atoe taarifa ya kukodisha sehemu hiyo katika mamlaka husika.

(2) Baraza litamtaka mkodishaji huyo kulipa asilimia tano (5%) ya pato ya kodi ikiwa ni ada ya ukodishaji wa sehemu hiyo.

(3) Endapo mkodishaji wa mnara atashindwa kulipa ada hiyo atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa asilimia ya pato la kodi na faini isiyopungua Shilingi Laki Moja za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Tatu za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita.

Ada ya ujenzi mnara na uendeshaji.

**29.-**(1) Baraza linamtaka mtu yeyote anayejenga, kuweka au kuhamisha mnara sehemu moja kwenda nyengine katika eneo kulipa Shilingi Milioni Tatu za Kitanzania.

(2) Mtu yeyote anayemiliki mnara wa mawasiliano katika eneo, atalipia ada ya uendeshaji wa mnara ambayo ni Shilingi Milioni Mbili na Laki Tano za Kitanzania kwa kila mwaka.

(3) Endapo mjenzi wa mnara huo atashindwa kulipa ada hiyo, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Mbili na isiyozidi Shilingi Milioni Tano au kutumikia kifungo kwa muda usiopungua miezi sita (6).

CamScanner

**JADWELI LA KWANZA**
**(Ada ya Usafi wa Mazingira, Ujenzi, Egesho Kituo cha Dalala)**
**[Chini ya kanuni 5(3)(6), 6(2), 9(2), 10(4)(6) na 21(4)]**

| MAENEO | AINA YA BIASHARA | KIWANGO (TZS) |
|---|---|---|
| **USAFI** | Vituo vya Mafuta | 600,000/= kwa mwaka |
| | Viwanda vikubwa vilivyosajiliwa na ZIPA | 600,000/= kwa mwaka |
| | Viwanda vidogo | 240,000/= kwa mwaka |
| | Maduka na ofisi | 50,000 /=kwa mwaka |
| | Gereji | 50,000/= kwa mwaka |
| | Nyumba au Kaya | 3,000/= kwa mwezi |
| | Hoteli kubwa | 1,250,000/= kwa mwezi |
| | Hoteli ndogo | 500,000/= kwa mwezi |
| | Nyumba ya kulala wageni | 250,000 /= kwa mwezi |
| | Huduma za kutapisha choo | 150,000 /=kwa trip |
| | Huduma ya choo | 500/=kwa siku |
| | Kuunganisha mitaro | 50,000 /=kwa Mwaka |
| | Ghala | 100,000 /=kwa mwaka |
| | Mikahawa | 50,000/= kwa Mwaka |
| | Usafi wa mazingira kwa wajasiriamali wadogo | 500/= kwa siku |
| **MAEGESHO** | Maegesho ya Magari | 1,000 kwa saa |
| | Maegesho ya Vespa, Pikipiki na Honda | 5,00 kwa saa |
| **KITUO CHA DALALA** | Usafirishaji wa abiria kwa daladala | 1000/=kwa siku |

CamScanner

**JADWELI LA PILI**
**(Ada ya Fomu ya Leseni)**
**[Chini ya kanuni 13, (2)(8) 14, 21(4), 22(3)(4), 23(4)(5)(6) na 24(3)]**

| HUDUMA | CHANZO CHA MAPATO | KIWANGO (TSH) |
|---|---|---|
| **FOMU** | Maombi ya leseni ya biashara | 10,000/= |
| | Maombi ya Leseni ya Nyumba za kulala wageni | 100,000/= |
| | Maombi ya bodaboda na bajaji | 2000=/ |
| | Maombi ya Ujenzi kuchukua fomu 3000/= | 10,000/= kurejesha |
| | Ukaguzi wa Afya | 10,000/= |
| | Ukaguzi wa lesen | 10,000/= |
| **MADUKA NA VIWANDA** | | |
| | **MTAJI** | **ADA YA LESENI** |
| | Isiyozidi 1,000,000 | 40,000/= |
| | Inayozidi 1,000,000 – 5,000,000 | 80,000/= |
| | Inayozidi 5,000,000 – 10,000,000 | 100,000/= |
| | Inayozidi 10,000,000 – 20,000,000 | 150,000/= |
| | Inayozidi 20,000,000 – 40,000,000 | 200,000/= |
| | Inayozidi 40,000,000 – 60,000,000 | 250,000/= |
| | Inayozidi 60,000,000 – 80,000,000 | 300,000/= |
| | Inayozidi 80,000,000 – 100,000,000 | 350,000/= |
| | Inayozidi 100,000,000 – 150,000,000 | 400,000/= |
| | Inayozidi 150,000,000 – 200,000,000 | 450,000/= |
| | Inayozidi 200,000,000 – 250,000,000 | 500,000/= |
| | Inayozidi 250,000,000 – 300,000,000 | 550,000/= |
| | Inayozidi 300,000,000 | 600,000/= |

CamScanner

| MALIASILI, DAGAA NA MWANI | | |
|---|---|---|
| **DAGAA** | Kiwanja | 15000/= kwa mwezi. |
| | Kibanda | 500,000/= kwa mwaka. |
| | Dagaa au unga wa dagaa | 2,000/= kwa roba |
| **MALIASILI** | Mkaa | 500/= kwa polo au gunia |
| | Nguzo au Miti | 2000/= kwa korja |
| | Fito | 500/= kwa mzigo |
| | Mbao | 500/= kwa ubao |
| **MWANI** | | Mwani 50,000/= kwa Roba |
| **BIASHARA NYENGINEZO.** | | |
| | Yadi za magari | 400,000/= |
| | Fundi ushoni vyarahani zaidi ya 3 | 60,000/= |
| | Huduma za simu wakala | 200,000/= |
| | Mikahawa midogo | 50,000/= |
| | Huduma za ofisi ndogo | 150,000/= |
| | Huduma za ofisi kubwa | 300,000/= |
| | Ghala dogo (chini ya 16 sqm) | 300,000/= |
| | Ghala kubwa (zaidi ya 16 sqm) | 500,000/= |
| | Huduma za mitandao | 100,000/= |
| | Gereji ndogo | 150,000/= |
| | Gereji kubwa | 400,000/= |
| | Kuosha vyombo vya moto | 200,000/= |
| | Kampuni zinazotoa huduma | 300,000/= |
| | Vitu chakavu (kachara) wadogo | 100,000/= |
| | Vitu chakavu (kachara) wakubwa | 200,000/= |
| | Kumbi za shughuli | 200,000/= |
| | Benki | 1,000,000/= |
| | Mashirika | 1,000,000/= |
| | Maduka ya kubadilishi fedha | 500,000/= |
| | Wakala wa Benki | 200,000/= |
| | Bekari | 150,000/= |

CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| | Wakala wa Usafirishaji na Uingizaji | 300,000/= |
| | Dobi wadogo | 150,000/= |
| | Dobi wakubwa | 250,000/= |
| | Saluni | 80,000/= |
| **BIASHARA NDOGO** | | |
| Wafanyabiashara wasio na maeneo maalum | Vitafunwa, mboga mboga, matunda, vyakula, samaki, vinywaji, mazao ya misitu, wauza mikate, wauza/waanika dagaa na biashara zinazofanana na izo | 30,000/= kwa mwaka |
| Wafanyabiashara katika maeneo maalum | Vitafunwa, mboga mboga, matunda, vyakula, Samaki, vinywaji, na biashara na huduma nyinginezo katika maeneo hayo maalumu | 100,000/= |

**ZIMETIWA** saini leo tarehe 6 Mwezi wa Juni , 2022

.........................................................
**CHUMU SHUWARI MACHANO**
**MEYA MAGHARIBI "A"**

.............................................
**MBARAKA SAID HASUNI**
**MKURUGENZI MAGHARIBI "A"**

**LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI - ZANZIBAR 2022**

CS CamScanner